Yesu akamwambia:

"Nitalijenga Kanisa langu"

Mathayo 16:18



Mafunzo juu ya Kanisa lake Yesu Kristo katika Maandiko Matakatifu.

Jean Manning
HUDUMA YA UVUVIO AUSTRALIA

YALIYOMO

AMRI

Yesu anafundisha kile tunastahili kufanya katika Injili

Sura ya Kwanza Yesu atalijenga kanisa Lake.
Sura ya Pili Yesu anawafunza Viongozi kuliongoza na kulijenga

MATENDO

“Matendo ya Mitume” ya twambia kile walifanya

Sura ya Tatu Mitume wanatii–Kanisa linachipuka

UFAFANUSI

Barua [Nyaraka] kutoka kwa mitume zinafanua namna na sababu ya matendo ya Kanisa
Sura ya Nne Kanisa – Mwili wa Kristo

Sura ya Tano Kanisa – Bibi-arusi wa Kristo

Utangulizi.

Kwa watu wengi, kanisa ni ule mjengo ambapo watu hukusanyika siuku ya Jumapili kwa ajili ya ibada yaa Mungu.

Katika funzo hili, tunaenda kujunguza Maandiko Matakatifu kuona na kuelewa kile ambacho Yesu alikiita Kanisa Lake, na jinsi alivyouthibitisha uongozi katika Kanisa Lake.

Tutakuwa tukilichunguza Neno la Mungu tukitafuta yale mambo ambayo Yesu atatumia katika kuliunganisha Kanisa Lake lenye mwili wa viungo vingi.

Tutakuwa tukijifunza muundo wa kanisa ambao Bwana alimfunulia Mtume Paulo, na tutambue tena Kanisa ambalo lilikuwa halisi katika jumuia katika Karne ya kwanza baada ya kufa na kufufuka kwa Bwana Wetu Yesu Kristo.

Tutakuwa tukichunguza miongozo ya namna Kanisa laweza kukomaa kufanyika “kanisa tukufu, lisilo na ila wala kunyanzi wala lo lote kama hayo; bali liwe takatifu lisilo na mawaa.” Efeso 5:27

Acha tutambue tena Kanisa la kweli ambalo lilikusudiwa kuwa Bibi-arusi wake Kristo – Kanisa ambalo “limejiweka tayari” kwa “arusi ya Mwana-Kondoo.” Ufunuo 19:7

Sura ya Kwanza.

YESU ATALIJENGA KANISA LAKE.

Yesu akasema:



"Mungu, ambaye alisema zamani na baba zetu katika manabii kwa sehemu nyingi na kwa njia nyingi, mwiso wa siku hizi amesema na sisi katika Mwana, aliyemweka kuwa mrithi wa yote, tena kwa yeye aliufanyea ulimwengu." Ebr. 1:1-2

Soma Ebrania 3:1-6

- Yesu ni Mjenzi

Ili tuweze kuelewa kanisa ni nini, tunahitaji "tumtafakari sana mtume na kuhani wa maungamo yetu, Kristo Yesu" (a.1), kwa "maana huyo amehesabiwa kuwa amestahili utukufu zaidi kuliko Musa, kama vile Yeye aitengenezaye nyumba alivyo na heshima zaidi ya hiyo nyumba". (a.3)

- Kanisa litajumuisha waamino na watakuwa milki yake.

Kwa hivyo tunamtafakari "Kristo kama Mwana juu ya nyumba ya Mungu; Ambaye nyumba yake ni sisi kama tukishikamana sana na ujasiri wetu na fahari ya taraja letu mpaka mwisho." (a.6)

- KANISA LITAJENGWA JUU YA IMANI.

Soma Mathayo 16:13-19.

Yesu alikuwa na Wanafunzi Wake alipowauliza:



Alisikia jawabu lao (a.14), kisha akawaambia:



Petro akajibu akasema: "Wewe ndiwe Kristo, Mwana wa Mungu aliye hai" (a.16).
Yesu alimbariki Petro na akwaambia wanafunzi kuwa jawabu hili ni ufunuo kutoka kwa Mungu, Baba Yake wa mbinguni. (a.17).

Yesu akasema:



Petro alikuwa amekiri tu kwamba Yesu ni Mwana wa Mungu aliye Hai.
Ni katika msingi huu wa imani ndani ya Yesu Kristo ambayo inakuja kama ufunuo kutoka kwa Mungu, kanisa litajengwa.
Ukristiano ni imani iliyofunuliwa.

Katika Maandiko Matakatifu Yesu Kristo anafahamika kama Mwamba.

> Kumbu kumbu 32:4 "Yeye Mwamba, kazi Yake ni kamilifu."
>
> Zaburi 95:1 "Tumfanyie shangwe Mwamba wa wokovu wetu."
>
> 1 Kor. 10:4 "wote wakanywa kinywaji kile cha roho; kwa maana waliunywea Mwamba wa roho uliowafuata; na Mwamba ule ulikuwa ni Kristo."

Mtume, Paulo anasema:

> Maana msingi mwingiine hakuna mtu awezaye kuuweka, isipokuwa ule uliokwisha kuwekwa, yaani, Kristo Yesu. 1 Kor. 3:11

YESU YUKO WAZI SANA ANAPOSEMA KUWA MSINGI WA KANISA UTAKUWA JUU YA IMANI NDANI YAKE KAMA MWANA WA MUNGU ALIYE HAI.

- KANISA LITAWAJUMUISHA WATU

Yesu alikuwa akimwambia Petro ambaye jina lake linamaanisha "jiwe dogo".
Petro alifanyika jiwe la ujenzi wa kanisa la kwanza ambalo Yesu atajenga.
Katika waraka wake, Petro anawaandikia waaminio:

> Ninyi nanyi, kama mawe yaliyo hai, mmejengwa mwe nyumba ya Roho. 1 Pet.2:5a

Hakika, kanisa sio jengo. Linajumuisha watu wanaoishi na ambao wanaungamanishwa vema kumfanyia Mungu maskani.
Neno "kanisa" katika Kiyunani ni "ekklesia" na linamaanisha "wale walioitwa au kusanyiko. [Strong's Concordance 1577]

Soma Efeso 2:19-22

- Waaminio ni "ni wenyeji pamoja na watakatifu, watu wa nyumbani mwake Mungu" (a.19)
- "Mmejengwa juu ya msingi wa mitume na manabii, naye Kristo Mwenyewe ni jiwe kuu la pembeni" (a.20)
- "katika yeye jengo lote linaungamanishwa vema na kukuwa hata liwe hekalu takatifu katika Bwana" (a.21)
- "Katika yeye ninyi nanyi mnajengwa pamoja kuwa maskani ya Mungu katika Roho." (a.22)

Watu ambao wameupokea ufunuo kutoka kwa Mungu kwamba YesunKristo ni Mwana wa Mungu aliye hai wanaitwa kutoka katika mawazo au nia ya mwili ya dunia na kujengwa pamoja kuwa nyumba ya Roho.

Mwanamke Msamaria alichanganyikiwa ni mahali gani anastahili kwenda kuabudu. Yesu akamfafanulia kuwa mahali sio swala muhimu kwa ajili ya ibada ya kweli.
Yesu akamjibu akamwambia:

> Lakini saa inakuja, nayo saa ipo, ambayo waabuduo halisi watamwabudu Baba katika Roho na Kweli; maana Baba awatafuta watu kama hao wamwabudu. Yohana 4:23

Kanisa ni Mwili wa kiroho. Linajumuisha watu walio na imani ndani yake Yesu Kristo.
Watu wa aina hii wametambua Maandiko Matakatifu kuwa Neno la Mungu na kulikubali:

- ✓ Kuwa Yesu, ambaye ni Neno, ananena ukweli maana ndiye "njia, ukweli na uzima." (Yohana 14:6)
- ✓ Kuwa Mungu atatupenda na aje afanye makao yake pamoja nasi tunapompenda Yesu na kuzishika amri zake. (Yohana 14:23)
- ✓ Kuwa kanisa ni Mwili wa Kristo na Yesu ndiye Kichwa (Efe. 1:22-23)

- KANISA AMBALO YESU ANAJENGA LITAKUWA NA MAMLAKA

Yesu akamwambia:

> Milango ya kuzimu haitalishinda. Math. 16:18

YESU ANATANGAZA KUWA NGUVU ZA UOVU HAZITAWEZA KUHARIBU KILE ANAJENGA.

Milango inawakilisha mamlaka ya kuzimu.
Yesu akamwambia:

> Nimepewa mamlaka yote mbinguni na duniani. Mathayo 28:18

Yesu aliwapa mamlaka ya kujenga watu wale aliofunza, kwa mitume Wake, na kuwatuma waende katika Jina Lake kuweka msingi wa kanisa Lake.

> ….. **watu wa nyumbani mwake Mungu, mmejengwa juu ya msingi wa mitume na manabii**, Efe. 2:20

Yesu alimpa funguo (ishara ya mamlaka) za ufalme wa mbinguni kwake Petro, wa kwanza katika mawe ya ujenzi wa kanisa Lake.

Akamwambia:

> Nami nitakupa wewe funguo za ufame wa Mbinguni

Mathayo 16:19



Hizo funguo zilifungua milango. "Aliye na ufunguo wa Daudi, Yeye mwenye kufungua wala hapana afungaye, naye afungaye wala hapana afunguaye." (Ufu. 3:7)

Alikuwa anawapa mitume wake mamlaka ya kuweka huru ama kufunga. Tutaona jinsi mamlaka haya yalivyotumika katika sura ya pili. (Yesu anawafundisha viongozi Wake)
Kama mtume wa Mwana-Kondoo, Petro alitumia fungukufungua njia katika ufalme Wayahudi Siku ya Pentekoste (Matendo 2:14-39), na Mataifa katika nyumba ya Kornelio (Matendo 10:34-43). Katika misimu yote miwili aliweka misingi ambayo iliweka imani katika mioyo ya wasikilizaji.

Baadaye mtume, Paulo, aliupokea ufunuo kuhusu muundo wa Kanisa la Yesu Kristo.

Alisema: "Maana sisi tu wafanyakazi pamoja na Mungu; ninyi ni shamba la Mungu, ni jengo la Mungu. Kwa kadri ya neema ya Mungu niliyopewa, mimi, kama mkuu wa wajenzi mwenye hekima, naliuweka msingi, na mtu mwingine anajenga juu yake. Lakini kila mtu na aangalie jinsi anavyojenga juu yake." (1 Kor. 3:9-10)

- <u>MWILI WA KRISTO UMEUNGANIKA NA KICHWA</u>

Yesu anakusudia kuwa Kanisa Lake hapa duniani (Mwili Wake) litaungamanika nay ale yanatendeka mbinguni (na Kichwa Chake), ambapo Yesu anatwala milele. Kutakuwa na uhusiano kati ya mwili wa watu hapa duniani na Kichwa (ambaye ni Kristo) mbinguni.

Kutakuwa na utawala uo huo (mamlaka) aliopewa Adamu juu ya kanisa (Mwanzo 1:28) na kuungamanika sawa sawa kayi ya mbingu na kanisa kama jinsi ilivyokuwa kati ya Adamu na Mungu. (Mwa. 1-3)

> Naye ndiye kichwa cha Mwili, yaani, cha kanisa; naye ni mwanzo, mzaliwa wa kwanza katika wafu, ili kwamba awe mtangulizi katika yote. Kol 1:18

Haya yote yatawezekana kwa sababu kanisa litakuwa limejengwa juu ya ufunuo wa kumjua Yesu alivyo.

- Yesu atakuwa msingi wa kanisa Lake (Mwamba)
- Yesu atakuwa kichwa cha kanisa Lake (Efe. 4:15)
- Yesu atakuwa mtangulizi juu ya Mwili Wake ambalo ni kanisa (Kol. 1:18)

Huu ufunuo ni wa kumrejesha mwanadamu katika uhusiano maridhawa na Mungu kwa njia ya sadaka ya Mwana Wake.

Wote wanaoukubali ushindi ambao Yesu alishinda kupitia kwa kifo Chake na kufufuka Kwake watatakaswa kutoka katika njia za dunia ili wawe kanisa lake Yesu Kristo.

Hawa watu wataunganika kama mwili wa Kristo Kwake Kristo ambaye ni Kichwa cha Kanisa Lake.

kutakuwa na uhai kanisani kwa sababu hawa "walioitwa kutoka katika watu" watakuwa wakiishi katika utii Kwake yeye aliye uzima.

Yesu akawaambia: Maneno hayo niliyowaambia ni Roho,tena ni uzima. Yohana 6:63

- Yesu ni Mjenzi, bali amepeana funguo na mipango kwa wake aliofundisha.
- Kanisa ni milki Yake. "Alilipenda Kanisa hata akajitoa kwa ajili yake". (Efe 5:25b)
- Kanisa ni makao ya Mungu katika Roho.
- Kanisa linataiwa kutawala duniani.

Hakuna mahali popote Yesu anazungumzia Kanisa Lake kama majengo. Anazungumzia juu ya watu wanaomuamini Yeye, wanaokaa katika uhusiano Naye na wale wanaomtii Yeye.

Kanisa ni watu wa Mungu walioitwa kutokawanaojulikana kama mwili wa Kristo na kuunganika na Yesu ambaye ni Kichwa cha Mwili Wake.

Kanisa Lake Kristo ni lile linaloenda katika utii wa ukweli wa Maandiko Matakatifu.

YESU ATALIJENGA KANISA LAKE, AMEONYESHA NJIA.

AMENENA UKWELI. AMETOA UHAI WAKE KWA AJILI YA KANISA.

AMESITAWISHA UONGOZI KATIKA KANISA LAKE.

Sura ya Pili

YESU ANAWAFUNZA VIONGOZI KWA AJILI YA KANISA LAKE

“Akapanda mlimani



Akawaita aliowataka mwenyewe.

wakamwendea.

Akaweka watu kumi na wawili,

- Wapate kuwa pamoja naye
- Na kwamba awatume kuhubiri,
- Tena wawe na amri ya kutoa pepo.” Mark 3:13-15

Luka anatwambia kuwa Yesu “aliwaagiza kwa Roho Mtakatifu wale mitume aliowachagua.” Matendo 1:2

- YESU ANAWAAGIZA WALE ALIOWACHAGUA

Mwanafunzi ni yule anayesoma. Yesu aliwahifadhi hawa watu pamoja Naye ili wajifunze kutoka Kwake . Walikuwa mashahidi kwa matendo makuu ya Mungu kupitia kwa maisha yake Yesu.

SomaMathayo10:2
Mathayo sasa anawaita wale Thenashara mitume.
Ni kwa hawa kumi na wawili Yesu alizingatia na kuwapa maelezo ili waweke misingi kwa ajili ya Kanisa Lake.

Aliwaambia:

- ✓ Kile watakacho hubiri. Mathayo 10:7
- ✓ Kile watafanya a.8
- ✓ Jinsi ya kuwatunza watu po pote walikoenda a.11-14
- ✓ Kile chha kusema a.19-20
- ✓ Jinsi ya kustahimili katika mateso a.21-23
- ✓ Alitarajia kujitolea kwao kikamilifu a.37-39

- YESU ALIUSITAWISHA UONGOZI WA KIMITUME KWA AJILI YA KANISA LAKE

Yesu akawaambia:

> Awapokeaye ninyi, anipokea mimi; naye anipokeaye mimi, ampokea yeye aliyenituma. a.40

Pale ambapo mitume walipokewa, Bwana atapokewa. Bwana atapata makao katika kanisa ambalo mitume wanapokewa.

Huu ndio ulikuwa muundo wa kusitawisha kanisa la Agano Jipya.

> Kanisa “juu ya msingi wa mitume na manabii” Efeso 2:20
>
> “Na Mungu ameweka wengine katika kanisa: wa Kwanza mitume”. 1 Korintho 12:28
>
> “Naye alitoa wengine kuwa mitume…..” Efeso 4:11

Hawa watu walishuhudia maisha ya maombi ya Yesu, utenda kazi wake kuhusiana na mapenzi ya Baba Yake na aina ya maisha Yake; aliwafunza, aliwafundisha na kuwatuma Yeye mwenyewe na Mamlaka Yake na kuwapa nguvu.

- YESU ANAFUNZA

  (i) Kikundi
  Katika Injili tunasoma kuwa wanafunzi “walimfuata” alipokuwa akienda huko na huko. (mfano Mark 6:1)
  Yesu alikuwa na kikundi cha watu waliokuwa pamoja naye po pote alipoenda.

  Walikuwa pamoja Naye Alipowaponya wagonjwa (Mathayo 9:18-25), wakati Alipowatoa pepo (Mathayo 8:28-34), wakati Alipowafufua wafu (Yohana11:1-34). Na wale aliowachagua, mitume Wake walikuwa mashahidi wa mambo haya. Haya ni baadhi ya mambo ambayo aliwatuma kwenda kufanya.

  > Akawaita wale Thenashara, akawapa uwezo na mamlaka juu ya pepo wota na kuponya maradhi.
  >
  > Akawatuma wautangaze ufalme wa Mungu, na kupoza wagonjwa . Luka 9:1-2

Alipowatuma, “Akawatuma wawili wawili wamtangulie kwenda kila mji na kila mahali alipokusudia kwenda mwenyewe.” (Luka 10:1)

Siku ya Pentekoste, Petro alitumia mamlaka ambayo Yesu alikuwa amempa (Mathayo 16:19) lakini “akisimama pamoja na wale kumi na mmoja, akapasa sauti yake, akawaambia……..” (Matendo 2:14)
Petro hakuwa pekee yake; alikuwa anawakilisha kikundi chote cha mitume ambacho Yesu alikuwa amefunza.

(ii) Katika Sala
Wanafunzi wake waliona jinsi alivyosali. (Marko 1:35)

Aliwafundisha jinsi ya kuomba (Mathayo 6:5-13), akiwaonyesha kuwa uhusiano na Mungu Baba ndio msingi wa sala zote.

Aliwafundisha malengo ya maombi, kuutafuta ufalme wa Mungu kwanza.

- Kumletea Mungu utukufu
- Kuomba ufalme wa Mungu uje
- Kuomba mapenzi yake yafanyike hapa duniani
- Kuomba chakula kutoka kwa Mungu, cha Roho na mwili.
- Tafuta msamaha na kusamehe
- Kuomba muongozo kupinga majaribu na ukombozi kutokana na yule muovu
- Kutambua kuwa Ufalme na nguvu ni wa Bwana

Alionya kuwa maisha bila maombi huongoza katika majaribu

> Kesheni, mwombe, msije mkaingia majaribuni; roho i raadhi, lakini mwili ni dhaifu. Mathayo 26:41

Aliwafunza kuomba kwa ajili ya watenda kazi kama jambo la umuhimu sana. (Mathayo 9:37-8)

(iii) <u>Aliwapatia ujuzi wa matendo</u>

Sma Yohana 6:5-11

> Basi Yesu akaitwaa ile mikate, akashukuru, akawagawia walioketi; na kadhalika katika wale samaki kwa kadri walivyotaka. v.11

(iv) <u>Aliwafuchulia Siri</u>

> Wala pasipo mfano hakusema nao; <u>lakini akawaeleza wanafunzi wake mwenyewe mambo yote kwa faragha</u>. Marko 4:34

Yesu akajibu akawaambia wanafunzi Wake:

> Ninyi mmejaliwa kuzijua siri za ufalme wa mbinguni, bali wao hawakujaliwa. Mathayo 13:11

Baadaye, mtume, Paulo, anazungumzia siri ambazo zimefunuliwa kwa mitume ambao sasa wanuleta ufunuo huo kwa kanisa.

> Kwa hayo, msomapo, mtaweza kuutambua ufahamu wangu katika siri yake Kristo. Siri hiyo hawakujulishwa wanadamu katika vizazi vingine; kama walivyofunuliwa mitume wake watakatifu na manabii zamani hizi katika Roho. Efe 3:4-5

(v) Yesu aliwapa wafuasi wake mamlaka

- Kuushinda uovu

Tazama nawapa amri ya kukanyaga nyoka na nge, na nguvu zote za yule adui, wala hakuna kitu kitakachowadhuru. Luka 10:19

- kufunga au kusamehe dhambi

Soma Mathayo 18:15-18
Hizi ni zile funguo ambazo alimpa Petro aliposema: "Nitalijenga kanisa Langu." (Mathayo16:19)

Yesu akawaambia:

Amin, nawaambieni, yo yote mtakayofunga duniani yatakuwa yamefungwa mbinguni, na yo yote mtakayofungua duniani yatakuwa yamefunguliwa mbinguni Mathayo 18:18

Hizi funguo zinawapa mitume haki ya kufungua watu kutoka kwa dhambi zao, au kuwahifadhi [kufunga] muumuni asiyetubu katika dhambi yake.

Soma Yohana 20:23 ambapo Yesu anatoa amri hii kuhusu msamaha wa dhambi au kuwaacha watu katika makosa yao.

- Kulijenga Kanisa Lake

Soma Mathayo 28:18-20



Yesu alimuomba Mungu,Baba yake, kwa ajili ya hao wanafunzi aliofunza:



Alisema kutakuwa na mamlaka katika makubaliano.



(vi) <u>Yesu aliahidi Roho Mtakatifu kuwatia nguvu wanafunzi wake</u>



Yesu alikuwa amewaahidi wanafunzi kuwa hatawaacha bila msaidizi (Yohana 14:18), na katika sura ya 14-16 ya injili ya Yohana tunasoma yale aliyofundisha kuhusu jukumu la Roho Mtakatifu katika maisha ya Yule aaminiye.

(vii) <u>Yesu aliwatuma wanafunzi wake kuwa mitume.</u>

Yesu aliwatokea wanafunzi wake baada ya kufufuka

Anawatuma:



Anawapa nguvu:



Anapeana mamlaka ya kusamehe dhambi au kuwaacha watu katika makosa yao:



KATIKA SIKU ZAKE YESU HAPA DUNIANI

- Aliinua na kikufunza kikundi
- Aliwapa mamlaka Yake kulithibitisha kanisa lake
- Aliwathihirishia mfano wa kanisa ambalo litathihirisha ufalme wa Mungu hapa duniani
- Aliahidi kumtuma Roho Mtakatifu kuwatia nguvu
- Aliwatuma watu 12 kuwa mitume kulithibitisha na kuongoza kanisa Lake

KUPITIA KWA HAO THENASHARA "MITUME WA MWANA-KONDOO" (UFUNUO 21:14) AMBAO ALIFUNZA, YESU ALIUWEKA MSINGI WA KANISA LAKE.

Sura ya Tatu

WANAFUNZI WANATII - KANISA LA AGANO JIPYA LAJITOKEZA

Ni muhimu kukumbuka kuwa wale Yesu alikuza kwa ajili ya kujenga kanisa Lake (yaani, mitume Wake) walikuwa na mafundisho ya Agano la Kale pekee yake na mafunzo ambayo Yesu aliwafundisha.

- Injili inatwambia yale Yesu alifanya na kufundisha.
- Kitabu cha Matendo ya Mitume chatuambia yale mitume na wanafunzi walifanya.

MISINGI ILIKUWA IMEWEKWA.

Luka anapoanza kuandika habari ya matendo ya mitume na kuchikpuka kwa kanisa, anatoa ujumbe mfupi lakini mkamilifu juu ya misingi ambayo tayari ilikuwa imewekwa kwa ajili ya kulijenga kanisa.

Soma Matendo 1:1-11 kama kumbu-kumbu ya misingi ambayo kanisa linatakiwa kukua juu yake.

- ✓ Matendo ya Yesu na mafunzo (a.1)
- ✓ Imani katika Ufufo Wake na kupaa (a.2)
- ✓ Alikuwa amewachagua na kuwafundisha mitume (a.2)
- ✓ Walikuwa na thibitisho kuwa hakika alifufuka kutoka kwa wafu (a.3)
- ✓ Aliwapa amri zake kwa njia ya Roho mtakatifu (a.2)
- ✓ Aliwaambia wangojee nguvu za Roho Mtakatifu (a.8)
- ✓ Roho Mtakatifu atawawezesha kuwa mashahidi wa Yesu – nyumbani, kisha maeneo ya mbali na hata "miisho yote ya dunia". (a. 8)
- ✓ Yesu atarudi tena (a.11)

UONGOZI ULITHIBITISHWA.

Hadithi ya mchipiko wa kanisa unajitokeza ukiwa na mitume na wandugu. Matendo 1:12-15



Kulikuwa na masharti ya kutekeleza.

Wakuchaguliwa alikuwa awe:

1. Yule aliyemfuata Yesu kutoka wakati wa ubatizo Wake hadi kwenda Kwake juu. Matendo 1:21-22

+

2. Yule ambaye ni shahidi wa ufufuo wa Bwana Wetu Yesu Kristo AMatendo 2:22

<u>Umuhimu wa uongozi wa kimitume</u>

Mtume wa Kumi na mbili alipochaguliwa

Hata ilipotimia Siku ya Pentekoste

walikuwako mahali pamoja

ROHO MTAKATIFU AKAJA



<u>WAAMINIO WAKAPATA NGUVU</u>

- Kukaja ghafla toka mbinguni, uvumi kama uvumi wa epepo wa nguvu ukienda kasi ukaijaza nyumba yote(a.2)
- Kukatokea ndimi zilizogawanyika kama ndimi za moto uliowakalia kila mmoja wao (a.3)
- Wote wakajazwa na Roho Mtakatifu (a.4)
- Wakaanza kusema kwa lugha nyingine (a.5)
- Watu watauwa wa kila taifa chini ya mbingu wakashikwa na fadhaa(a.5)

Ahadi ya Baba (Luka 24:49) iliyotelewa na Yesu imewadia!

<u>KANISA LINAZALIWA</u>

Petro, “akiwa amevikwa uwezo kutoka juu”, akasimama“ pamoja na walekumi na mmoja” (Matendo 2:14) na kuhubiri kuhusu kutimia kwa unabii ambao Yesu alikuwa ametoa na watu wapatao elfu tatu “wakafunguliwa” katika ufalme wa mbinguni siku hiyo.

Hao watu elfu tatu wakauliza:

Tutendeje, ndugu zetu? Matendo 2:37

Petro aliwapa mambo matatu (a.38)

Tubuni

Mkabatizwe

Pokea kipawa cha Roho Mtakatifu



Sasa kuna 3000 + 120 waliokuwa wakingoja pamoja katika maombi.

WALIFANYA NINI?

Soma Matendo 2:42

- ✓ Walidumu katika fundisho la mitume
- ✓ Walishiriki pamoja
- ✓ Waaliumega mkate
- ✓ Walisali

Fundisho la mitume

Mitume walikuwa wakifundisha na kutenda yale Yesu alikuwa amewafunza kufanya. (a.43)

 Ajabu nyingi na ishara.

Mitume na manabii wamepewa ufunuo

> ***Kwa kufunuliwa nalipokea siri hiyo ……. Siri hiyo hawakujulishwanadamu katika vizazi vingine kama walivyofunuliwa mitumw watakatifu na manabii zamani hizi katika Rohos. Efe. 3:3-5***

Ushirika

"Walikuwa na vitu vyote shirika, wakauza mali zao, na vitu vyao walivyokuwa navyo, na kuwagawia watu wote kama kila mtu alivyokuwa na hajawakishiriki chakula chao kwa furaha na kwa moyo mweupe". (v.44-46)

"wala hapakuwa na mtu mmoja miongoni mwao mwenye mahitaji; kwa sababu watu wote waliokuwa na viwanja au nyumba waliviuza, wakaileta thamani ya vitu vile vilivyouzwa, wakaiweka miguuni pa mitume; kila mtu akagawiwa kwa kadri alivyohitaji." Matendo 4:34-35

Kutoka kwa waraka wa Paulo kwa Wakorintho, tunafahamu kuwa walikula vyakula pamoja.
1 Kor 11:17-22

Kuumega mkate

Kila siku na kwa moyo mweupe, waliumega mkate pamoja kutoka kwa nyumba hadi nyumba. (a.46)

Kupitia kwa matendo haya, kulikuwa na hakikisho kuwa Yesu alikuwa akikumbukwa kila siku. Lazima kuwe kulikuwa na ufunuo wa Yesu, Kristo, katika kuumega mkate (Luka 24:30-31) maana Bwana alizidisha kanisa kila siku kwa wale waliokuwa wakiokolewa. (a.47)

Kusali

Kama jinsi tulivyoona awali, umoja na uvumilivu katika maombi ulileta kuja kwake Roho Mtakatifu. Kitabu cha Matendo ya Mitume kinanukuu matukio mengi kutokana na ushirika wa Maombi. Kwa mfano:

- ✓ Petro na Yohana walikuwa wakikwea pamoja kwenda hekaluni, saa ya kusali. Matendo 3:1
- ✓ Baada ya hao kuachiliwa kutoka gerezani, Petro na Yohana walienda mahali ambapo waaminio walikuwa wamekusanyika kwa maombi. Matendo 4:23-31
- ✓ Maamuzi yalifanywa baada ya mda katika maombi. Matendo 6:6
- ✓ Mitume walijitenga wenyewe, wakisema "na sisi tutadumu katika kuomba". Matendo 6:4
- ✓ Petro alienda kwa nyumba ya Mariamu ambako "watu wengi walikuwa wamekutana humo wakiomba". Matendo 12:12
- ✓ Kule Filipi, Paulo na Timotheo "walienda nje ya lango, wakaenda kando ya mto ambapo tukadhani ya kuwa pana mahali pa kusali.". Matendo 16:13

KANISA LILIKUTANIKA WAPI?

Mbeleni, "siku zote walikuwa wakidumu kwa moyo mmoja ndani ya hekalu, na kuumega mkate nyumba kwa nyumba .". Matendo 2:46

(i) Ndani ya hekalu

- Waliendelea na desturi ya dini ya Kiyahudi na wakautanika ndani ya hekalu kuomba mara nyingi katika Ukumbi wa Suleimani, na walikuwa wakialikwa katika masinagogi. (Matendo 17:2, 18:4, 19:8)

Mda si mda wakajulikana kama watu wa Njia hii, dini ya Wayahudi (Matendo 9:2, 24:14) mateso yaliwafanya waondoke katika masinagogi. Hapakuwa na mijengo maalum kwa ajili ya mikutano yao.

(ii) Nyumba kwa nyumba

- Hata hivyo, kutoka Siku ya Pentekoste, kanisa lilipoanzishwa, mikutano pia ilifanywa katika Nyumba za wapendwa.

Waliumega mkate nyumbani Matendo 2:46

Mikutano ya maombi ilikuwa nyumbani. Matendo 12:12

Ushirika ulikuwa nyumbani. Matendo 16:40,21:8

Mafunzo yalikuwa kutoka nyumba hadi nyumba. Matendo 20:20

Mataifa waliisikia habari njema ya Yesu Kristo na wakapokea Roho Mtakatifu katika nyumba ya Kornelio.Matendo 10:24-48

Mlinzi wa gereza huko Filipialiamini Mungu pamoja na nyumba yake. Matendo 16:34

Naye Paulo akakaa mda wa miaka miwili mizima katika nyumba yake aliyokuwa ameipanga, akawapokea watu wote waliokuwa wakimwendea, akihubiri habari za ufalme wa Mungu, na kuyafundisha mambo ya Bwana Yesu Kristo kwa ujasiri mwingi, asikatazwe na mtu. Matendo 28:31

Mateso yalisababisha kutwanyika

Kama vile wafuasi walivyoitwa dini, waliteswa na kuondolewa katika masinagogi.Matendo 22:4-5 Nyingi ya salamu zake Paulokatika nyaraka zake ziliandikiwa makanisa yaliyokuwa yakikutana katika nyumba, mfano: Warumi 16:5,10,11,14,15; 1 Kor 16:19.

Hakuna mahali po pote kunatajwa jingo ambalo lilikuwa limejengewa eti kanisa.

WALIITWA NANI?

- Mbeleni walikuwa tu waumini ya kiyahudi, walioitwa Njia, dini ya wayahudi.
- Kisha Neno la Bwana likawafikia mataifa, kukawa na Kanisa la Kataifa.

- Kule Antiokia, Wayahudi pamoja na Mataifa wanakuja pamoja "na wanafunzi kwa mara ya kwanza wakaitwa Wakristo kule Antiokia". Matendo 11:26

WATU WALIOAMINI WALIWAPENDEZA WATU WOTE

Kukawa na ajabu Nyingi na ishara. Hakuna aliyekuwa na hitaji – wote walikuwa na vitu shirika.

Kila mtu akaingiwa na hofu, ajabu nyingi na ishara zikafanywa na mitume Matendo 2:43	Walikuwa na vitu vyote shirika, wakauza mali zao, na vitu vyao walivyokuwa navyo, na kuwagawia watu wote kama kila mtu alivyokuwa na haja. Matendo 2:44-45

Hili lilikuwa kanisaa (a.47)

Wakimsifu Mungu	na	Kuwapendeza watu wote

HUDUMA ZINACHIPUKA

Vile waaminio walivyoendelea kubatizwa katika kanisa la Yesu Kristo, kulihitajika wanafunzi zaidi kwa ajili ya kazi ya kuwashughulikia waaminio wengine.

- ✓ Petro anakuwa mtume kwa Wayahudi, na Paulo kw Mataifa
- ✓ Yakobo analiongoza kanisa Yerusalemu
- ✓ Timotheo, Tito na Barnaba wanakuwa Mitume kuliweka kanisa katika mpango katika miji na sehemu zingine nje ya Yerusalemu
- ✓ Stefano na Filipo pamoja na wengine wanekuwa wasaidizi wa kuhudumu mezani
- ✓ Wengi wanaanza kuinuliwa katika shirika zilizikuwa nyumbani
- ✓ Waalimu wanachipuka. Juda, anayejiita mwenyewe kama mtumwa wa Bwana, anayaleta mafunzo ka kanisa
- ✓ Filipo anakuwa muinjilisti mkuu, na binti zake wanjulikana kama manabii
- ✓ Agaba anakuwa nabii miongoni mwa wengine wengi

KANISA AMBALO YESU ALIKUWA AMSITAWISHA LINAJITOKEZA

- ➢ Likiongozwa na mitume ambao yesu alichagua, pamoja na wale aliowachagua baada ya kupaa.
- ➢ Wanakutana kutoka nyumba hadi nyumba
- ➢ Wakiwa na lengo kuu la maombi
- ➢ Wakiwa wamejitolea na kudumu katika mafundisho
- ➢ Kuumega mkate na ushirika yalikuwa mambo makuu katika mikutano
- ➢ Maajabu na ishara zikiwa nyingi
- ➢ Likiwapendeza watu wote
- ➢ Likijuisha Wayahudi na Mataifa
- ➢ Wanaoitwa Wakristo

"Na wale wakatoka, wakahubiri kote kote, Bwana akitenda kazi pamoja nao, na kulithibitisha lile Neno kwa ishara zilizofuatana nalo." Marko 16:20

Sura ya Nne

Sura ya nne

KANISA – MWILI WA KRISTO

Kitabu cha Matendo ya mituma kimefichua kile ambacho mitume na wanafunzi walifanya kanisa lilipojitokeza.

Nyaraka (Barua) kwa makanisa na waaminio yatuonyesha muundo wa kujenga na jinsi ya kulileta kanisa katika ukamilifu.

Paulo, akiwaandikia Waefeso, anatoa picha ya kanisa likiwa ndani ya Kristo katika ulimwengu wa Roho, likikomaa jinsi linavyoenda na Bwana na mwishowe kuweza kusimama katikati ya upinzani.

Katika nyaraka zingine, Paulo, Petro, Yakobo na Juda wanasahihisha makosa ambayo kanisa limefanya kwa kuiacha njia ya kweli na kurudia matendo ya dini na matendo yanayokubalika na watu, pamoja na kuleta sheria katika njia za haki.

Katika nyaraka hizi, Kristo anapewa ukuu kama Kichwa cha Kanisa na kaniza linajulikana kama mwili wa Kristo.

KRISTO – KICHWA

"Akavitia vitu vyote chini ya miguu yake, akamweka awe Kichwa juu ya vitu vyote kwa ajili ya kanisa; ambalo ndilo mwili wake, ukamilifu wakeanayekamilika kwa vyote katika vyote."
Efeso 1:22-23

"kanisa liko chini yake Kristo." Efeso 5:24

- Kukua kunatoka kwa Kichwa

Kanisa linatakiwa "kukua hata kumfikia yeye katika yote, yeye aliye kichwa, Kristo,
Katika yeye mwili wote ukiungamanishwa na kushikanishwa kwa msaada wa kila kiungo, kwa kadri ya utendaji wa kila sehemu moj moja, huukuza mwili upate, kujijenga wenyewe katika upendo." Efeso 4:15-16

Kanisa linatakiwa kushikanishwa "kwa Kichwa, ambacho kwa yeye mwili wote ukiruzukiwa na kuungamanishwa kwa viungo na mishipa, hukua kwa maongeo yatokayo kwa Mungu." Kol 2:19

- Kristo kama Kichwa na ni mtanglizi juu ya Kanisa Lake

"Naye ndiye Kichwa cha mwili, yaani, cha kanisa; naye ni mwanzo, ni mzaliwa wa kwanza katika wafu, ili kwamba awe mtangulizi katika yote." Kol 1:18

- Kristo alilipenda Kanisa naaklisafisha akalitenga ili liwe takatifu

"alilipenda kanisa hata akajitoa kwa ajili yake, ili makusudi alitakase, na kulisafisha kwa maji katika Neno apate kujiletea kanisa tukufu." Efeso 5:25-27

KANISA NI MWILI WA KRISTO

Soma 1 Kor. 12:13-28
Paulo anatooa picha ya kanisa linavyofanya kazi kama mwili wa mwanadamu kila sehemu akiwa ma jukumu maalum kwa ajili ya mwili kufanya kazi yake ipasavyo.

Ni mwili mmoja
a:12 una viungo vingi, na viungo vyote vya mwili ule, navyo ni vingi, ni mwili mmoja; vivyo hivyo na Kristo.
a.13 sote tumebatizwa katika mwili mmoja

Kanisa lina viungo vingi
a.14 kwa maana mwili sio kiungo kimoja, bali ni vingi

Mungu amevitia viungo kila kimoja katika mwili kama alivyotaka
a.18 Bali Mungu amevitia viungo kila kimoja katika mwili kama alivyotaka

Kusiwe na faraka katika mwili
a.25 kusiwe na migawanyiko katika mwili

Mtume, Paulo, analisahihisha kanisa la Wakorintho katika 1 Kor. 1:11-13, akiwakumbusha kuwa kusiwe na migawanyiko katika mwili wa Kristo.

Je! Kristo amegawanyika?
1 Kor. 1:13

Matokeo yatakuwa:
a.26 kiungo kimoja kikiumia, vyote huumia nacho, na kiungo kimoja kikitukuzwa, viungo vyote hufurahi pamoja nacho.

Viungo kila kimoja pekee yake
a.27 ninyi mmekuwa mwili wa Kristo, na viungo kila kimoja peke yake.

Mtume, Paulo, anakumbusha kanisa la Korintho kuwa ni wajibu wa kila kiungo au mshiriki kuwa tayari kuchangia katika ushirika.

Basi, ndugu, itakuwaje? Mkutanapo pamoja, kila mmoja ana zaburi, ana fundisho, ana ufunuo, ana lugha, ana tafsiri. Mambo yote nayatendeke kwa kusudi la kujenga. 1 Kor.14:26

Mungu amepeana majukumu kanisani

a.28 Na Mungu ameweka wengine kanisani: wa kwanza mitume, wa pili manabii, wa tatu waalimu, kisha miujiza, kisha karama za kuponya wagonjwa na masaidiano, na maongozi, na aina za lugha.

MPANGO WA MUNGU KATIKA KANISA LA YESU KRISTO

- Kulingana na vile Mungu ameweka majukumu kanisani 1 Kor. 12:28

(i) mitume (ii) manabii (iii) waalimu (iv) miujiza
(v) masaidiano (vi) maongozi (vii) aina za lugha

- Kulingana na vile Bwana aliyefufuka Yesu Kristo ametoa kwa kanisa. Efeso 4:11

"Naye alitoa wengine kuwa mitume, na wengine kuwa manabii, na wengine kuwa wainjilisti, na wengine kuwa wachungaji na waalimu."

- Kulingana na misingi aliyowekwa na Bwana Yesu Mwenyewe.

Soma Efeso 2:19-22



- YESU KRISTO NDIYE KICHWA CHA KANISA
- WANAOAMINI WANAJUMUISHA KANISA – MWILI WA KRISTO
- MWILI WA KRISTO UNAUHUSIANO NA KICHWA
- MWILI UNAPENDWA, UNATAKASWA, UNASAFISHWA KUTOKA KWA KICHWA
- KUKUA KWA KANISA HUTOKA KWENYE KICHWA
- MUNGU AMEPEANA MAJUKUMU KANISANI
- KILA AAMINIYE NI KIUNGO PEKE YAKE KATIKA KANISA LA KRISTO, LILILOANDALIWA NA MUNGU

Sura ya tano

KANISA – BIBI-ARUSI

Katika uhusiano na Kristo

Mtume, Paulo, anatupatia pichaya kanisa lililo na uhusiano na Kristo, Mwenyewe, kama mke navyokuwa katika uhusiano na mumuwe.

Anaonyesha malezi kwa kanisa Lake jinsi anavyo tarajia mme amjali na kumtunza mkewe.

Yesu Kristo – Bwana - arusi

Yohana, mbatizaji alimfananisha Yesu na Bwana-Arusi. Akasema
"aifurahia sana sauti yake Bwana arusi". Yohana 3:29

Yesu anajitambua kama Bwana arusi waka wanafunzi wake Yohana walipomuuliza kuhusu kufunga. Alitabiri kuhusu kifo Chake na kuondoka. Mathayo 9:15

Kanisa – Bibi-arusi

Soma Efeso 5:22-32

- Kanisa linamtii bwana
- Kristo ndiye kiongozi wa kanisa
- Yeye ndiye Mwokozi wa Mwili
- Kanisa linamtii Bwana kwa kila jambo
- Kristo alilipenda kanisa na akajitoa kwa ajili yake
- Alitakasa kanisa na kulisafisha kwa maji ya Neno
- Kristo alifanya hivyo iliajitwalie kanisa tukufu, takatifu lisilo na mawaa
- Bwana anautunza Mwili Wake, kanisa

Kuzaa matunda

Paulo anatukumbusha katika Warumi 7:4 kwamba kanisa limekufa kwa ajili ya matendo ya sheria ambayo analinganisha na mme wa kwanza wa waumini wa Kiebrania.
Tunapoifilia sheria na kuanza kuishi kwa neema katika Agano Jipya lililoyolewa na Yesu kupitia kwa kumwagika kwa damu Yake, tunaolewa "na mwingine".

> Kadhalika, ndugu zangu, ninyi pia mmeifia torati, kwa njia ya mwili wa Kristo, mpate kuwa mali ya mwingine, yeye aliyefufuka katika wafu, kusudi tumzalie Mungu matunda –Warumi 7:4

"Kusudi tumzalie Mungu matunda."

Paulo anatumia picha hii kulikumbusha kanisa kuwa kunatakiwa kuzaa matunda katika maisha ya Mkristo kama jinsi ndoa ilivyo kati ya mme na mke wanavyozaa watoto.

Hakutakuwa na matunda ya waaminio wapya, kutakuwa pia na ushahidi wa maisha yaliyobadilika kwa sababu ya uhusiano kati ya kanisa linaloamini na Bwana.

<u>Bibi-arusi anagojea kwa matarajio kwa ajili ya kuja kwake Bwana arusi</u>
Yesu anawaonya wanafunzi wawe tayari kwa ajili ya kurdi Kwake.



Yesu ameiacha ahadi yake kuwa atawarudia wale walio Wake.



Yesu anafundisha mfano wa wanawali kumi walimngoja Bwaba arusi.

Soma Mathayo 25:1-13

Hawa wanawali kumi ni kama kanisa linalongoja kurudi Kwake Bwana Yesu Kristo

- Wote walingojea; wote walitoka kwenda kulaki Bwana arusi. a.1
- All had lamps – all had received the light of the knowledge of Christ. v.3
- Ni wachache tu walikuwa tayari na mafuta ya ziada – ni wachache walitembea katikaka nguvu za Roho Mtakatifu.a.3-4
- “lakini Bwana arusi alipochelewa, wote walisinzia wakalala.” a.5
- Usiku wa manane sauti ikasikika kuwa Bwana arusi anakuja. a.7
- Waliokuwa hawakujiandaa sawa, walifungiwa nje. a.10
- Bwana arusi akasema: “siwajui ninyi” kwa wale wasiokuwa tayari, ambao hawakuenda katika uhusiano naye. a.12

Kanisa kama Bibi arusi wake Kristo linatakikana lijitayarishe kwa ajili ya kurudi kwake Bwana.

- Wote wamepokea nuru ya maarifa yake Kristo
- Wote wanajua analirudia kanisa Lake
- Yesu anawatarajia hawa kutembea katika uhusiano pamoja naye

<u>Bibi arusi amejiandaa- wa utukufu</u>
Soma Ufunuo 21:2
Yohana anapokea ufunuo juu ya Bibi arusi wa Kristo kama mji mtakatifu, Yerusalemu Mpya.

- Ukishuka kutoka mbinguni.

Wakati tunapozaliwa mara ya pili, ama kutoka juu, tunaingia katika ufalme huu wa mbinguni. Paulo anawatia moyo Wakolosai 3:2 kwamba “Yafikirini yaliyo juu, siyo yaliyo katika nchi.”

- Umetayarishwa kama Bibi arusi aliyekwisha kupambwa kwa mumewe.

Katika waraka wake kwa makanisa, Paulo anatoa maagizo mengi juu ya kile tunatakiwa “kuvua” (Kol 3:8-11) na kile tunatakiwa “kuvaa”(Kol 3:12-14) ili tujitayarishe kwa ajili ya kurudi Kwake Bwana.

Paulo anaandika:



Soma Ufunuo 21:9-27
Yohana anpewa ufunuo zaidi juu ya Bibi arusi wa Kristo.



MKE WA MWANA-KONDOO

YOHANA ANAONYESHWA MJI MKUU, MJI MTAKATIFI YERSALEMU, UKISHUKA KUTOKA MBINGUNI KWA MUNGU. a.10

- UKIWA UMEJAA UTUKUFU WAKE MUNGU NA WA MWANA-KONDOO. a.11, 23
- UMEJAA NURU a.11, 23
- KULIKUWA NA MILANGO YENYE MAJINA KUMI NA MAWILI YA MAKABILA YA WANA WA ISRAELI

a.12 na Mngu alikuwa amethibitisha Agano Lake la Ahadi na makabila kumi na mawili ya Israeli; kanisa linatakiwa kutembea katika urithi wake.

- KULIKUWA NA MAWE YA MISINGI NA MAJINA YA MITUME WA MWANA-KONDOO YALIANDIKWA KWAKE.

a.14 kanisa limejengwa juu ya msingi wa mitume na manabii. (Efeso 2:20)

- MILANGO YA HUO MJI I HAIFUNGWI. a.25
- NA NDANI YAKE HAKITAINGIA CHO CHOTE KILICHO KINYONGE. a.27
- BALI WALE WALIOANDIKWA KATIKA KITABU CHA UZIMA CHA MWANA-KONDOO. a.27

****

NA ROHO NA BIBI-ARUSI WANASEMA, “NJOO!,” NAYE ASIKIAYE NA ASEME, ”NJOO!” Ufunuo 22:17

YEYE MWENYE KUYASHUHUDIA HAYA ASEMA, NAAM; NAJA UPESI. AMINA; NA UJE, BWANA YESU! Ufunuo 22:20